**HOTUBA YA MWENYEKITI WA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI MHE. JAJI (R) SEMISTOCLES S. KAIJAGE KATIKA MKUTANO WA TUME NA VIONGOZI WA VYAMA VYA SIASA UNAOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA MWL NYERERE JIJINI DAR ES SALAAM TAREHE 5 MACHI, 2019**

- **Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi,**
- **Waheshimiwa Wajumbe wa Tume,**
- **Mheshimiwa Msajili wa Vyama vya Siasa,**
- **Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,**
- **Mwakilishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu,**
- **Ndugu Mkurugenzi wa Uchaguzi,**
- **Mkuu wa Jeshi la Polisi,**
- **Watendaji wa Tume,**
- **Waandishi wa Habari,**
- **Mabibi na Mabwana.**

*Bwana Asifiwe!!!, Tumsifu Yesu Kristu!!!, Mwanakondoo Ameshinda!!!, Assalam Aleykum!!!.*

**Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, nitumie fursa hii kuwakaribisha nyote katika mkutano huu. Natambua kuwa pamoja na kwamba mna majukumu mengi lakini mmeitikia wito wetu. Tume inathamini sana uwepo wenu kwa kuwa ni sehemu ya mafanikio ya kile tulichokusudia kuzungumza siku ya leo.

Wote tunafahamu kuwa nchi yetu ipo katika maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Katika maandalizi hayo, Tume chini ya Ibara ya 74(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imepewa mamlaka ya kutekeleza majukumu mbalimbali ya msingi ikiwa ni pamoja na jukumu la kusimamia na kuratibu Uandikishaji wa Wapiga Kura katika uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na uchaguzi wa Madiwani kwa Tanzania Bara.

Kifungu cha 15(5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, sura ya 343 na kifungu cha 21(5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa Sura ya 292, Tume inapaswa kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mara mbili katika Uchaguzi Mkuu mmoja na Uchaguzi Mkuu mwingine unaofuatia. Napenda kuwataarifu kuwa, Tume inaendelea na maandalizi ya uboreshaji wa Daftari, ambapo mpaka sasa tayari imekamilisha baadhi ya michakato kama vile uhakiki wa vituo vya kujiandikisha, maandalizi ya vifaa vya uboreshaji wa Daftari, mkakati wa Elimu ya Mpiga Kura, nk.

**Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Zoezi la uhakiki wa vituo lililenga kuona kama kuna haja ya kuongeza vituo katika baadhi ya maeneo, kuona kama vituo vilivyopo bado vinakidhi matakwa ya kisheria na kufanya marekebisho mengine kama vile kubadilisha majina ya vituo au kurekebisha majina ya vituo yaliyokosewa.

Matokeo ya ukakiki huo kwa Tanzania Bara yanaonesha kuwa vituo vya kuandikisha Wapiga Kura vimeongezeka kutoka vituo 36,549 vilivyotumika kuandikisha Wapiga Kura mwaka 2015 hadi vituo 37,407. Vituo 6,208 vimebadilishwa majina na vituo 817 vimehamishwa kutoka Kijiji/Mtaa mmoja kwenda mwingine. Aidha, vituo 19 vimehamishwa kutoka Kata moja kwenda Kata nyingine. Matokeo ya uhakiki wa vituo vya kuandikisha Wapiga Kura kwa Tanzania Zanzibar yanaonesha kuwa vituo vimeongezeka kutoka 380 hadi vituo 407.
Aidha, wadau wetu watapewa orodha ya vituo vya kuandikisha Wapiga Kura kabla ya kuanza kwa zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Kwa upande wa vifaa kwa ajili ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, mchakato wa kupata vifaa vya kukarabati mashine za BVR umekamilika. Kinachosubiriwa ni kuvifanyia majaribio ya Uandikishaji katika kata mbili za, Kihonda iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na Kata ya Kibuta iliyopo katika Hamashauri ya Wilaya ya

Kisarawe. Imekuwa ni kawaida kabla ya kuanza rasmi kwa zoezi kubwa la uandikishaji, kufanya majaribio ili kuona namna na jinsi vifaa vya uandikishaji vinavyofanya kazi katika mazingira tofauti, lengo likiwa ni kupata na kuwa na namna bora ya kufanikisha zoezi hili.

Tume pia imejipanga kutoa Elimu ya Mpiga Kura kwa njia mbalimbali ikiwemo kutumia vyombo vya habari, machapisho mbalimbali, mitandao ya kijamii, gari la matangazo na kushirikisha wadau kwa kutoa vibali kwa asasi za kiraia ili zishiriki kutoa Elimu ya Mpiga Kura.

Maandalizi mengine yaliyofanyika katika kipindi hiki ni uchapishaji wa miongozo mbalimbali kwa wadau, ikiwemo ile ya Elimu ya Mpiga Kura na maelekezo ya zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, kwa watendaji na wadau wa uchaguzi vikiwemo vyama vya siasa.

Hizo ni baadhi tu ya hatua ambazo Tume imefikia katika maandaizi yake. Siku chache zijazo tutakutana nanyi tena kwa ajili ya kupeana taarifa kwa kina juu ya zoezi la uboreshaji ikiwemo ratiba ya zoezi hilo kwa nchi nzima, mfumo na taratibu zitakazotumika katika zoezi hilo.

**Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Sheria za Uchaguzi zimeipa mamlaka Tume kuandaa Kanuni mbalimbali zinazohusu michakato ya uchaguzi, Kifungu cha 124 (1) na Kifungu cha 12(6) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 na kifungu cha 125(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa Sura ya 292, vinaipa mamlaka Tume ya kuandaa kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Pamoja na kupewa mamlaka hayo kisheria, Tume imejiwekea utaratibu wa kuwashirikisha wadau katika hatua mbalimbali za uchaguzi, kwa lengo la kuhakikisha inajenga na kutekeleza misingi ya kidemokrasia katika kusimamia, kuratibu na kuendesha chaguzi zilizo huru, wazi, za haki na za kuaminika.

Madhumuni ya kukutana kwetu leo ni kuwafahamisha kuwa Tume imekamilisha jukumu lake la kuhuisha na kuboresha kanuni ambazo ziliandaliwa chini ya sheria hizo mbili mwaka 2008. Tume imeona ni vema ikawapitisha katika kanuni hizo kwa kuangalia yale maeneo ambayo yamefanyiwa marekebisho ama, kwa kuondoa au kuongeza vifungu lakini pia kuelezea sababu za marekebisho hayo.

Ni imani ya Tume kuwa kushiriki kwenu na kuelewa Kanuni hizi ni sehemu ya kufanikisha zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Kupitia mkutano huu Tume itapokea maoni na ushauri

kutoka kwenu kwa lengo la kujenga na kuimarisha ushirikiano nanyi wadau wetu wakuu, katika hatua hii ya mwanzo kabisa kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Mwaka, 2020.

**Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Ningependa nitumie fursa hii tena kuwashukuru kwa dhati kabisa kwa namna ambavyo mmekuwa mkitoa ushirikiano kwa Tume wakati wote, na niwaombe muendelee kutoa ushirikiano huo. Nasi Tume tutaendelea kutoa ushirikiano wakati wote wa utekelezaji wa shughuli za kiuchaguzi kwa mujibu wa Katiba, Sheria, Kanuni na Taratibu.

**Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

Kwa kumalizia, nirudie tena kuwashukuru wote kwa kuacha shughuli zenu muhimu na kuja kuhudhuria mkutano huu. Hii inaonyesha ni kwa kiasi gani mko tayari kushirikiana nasi katika kufanikisha michakato mbalimbali ya uchaguzi, ikiwa ni pamoja na katika hili linalotarajiwa kuanza hivi karibuni la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la wapiga Kura.

Baada ya kusema hayo, naomba kutamka kwamba **MKUTANO WETU UMEFUNGULIWA RASMI.**

*ASANTENI KWA KUNISIKILIZA*